HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

TAARIFA YA HALI YA WILAYA

1.0 UTANGULIZI:

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ipo kusini mwa mkoa wa Tanga kwa nyuzi za latitude 4^0 $9^{'}$ – 6^0 $0^{'}$ kusini mwa Ikweta na longitude nyuzi 36^0 $8^{'}$ – 38^0 $5^{'}$ mashariki mwa ‘‘Greenwich’’. Kwa upande wa Mashariki Wilaya ya Handeni inapakana na Wilaya za Pangani na Muheza, upande wa Kaskazini inapakana na Wilaya za Korogwe na Simanjiro, upande wa Magharibi inapakana nz Wilaya ya Kilindi na upande wa Kusini inapakana na Wilaya ya Bagamoyo.

1.1 ENEO:

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ina eneo la Kilometa za Mraba 6,453 (Ha.637,925.15). Eneo hili ni sawa na asilimia 23.59 ya eneo lote la Mkoa wa Tanga

HALI YA WILAYA (PHYSICAL FEATURES) NA HALI YA HEWA:

Kwa ujumla Halmashauri ya Wilaya HANDENI imegawanyika katika Kanda Kuu mbili nazo ni:-

(i) Ukanda wa Juu (Miinuko na Milima michache):

Ukanda huu unaundwa na miinuko ya milima iliyotawanyika na vilele vya milima ambayo mwinuko wake ni kuanzia meta 600 hadi meta 1,200 kutoka Usawa wa Bahari na umechukua karibu asilimia 75 (4,839.75 km^2) ya eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. Kiasi cha wastani wa mm800 – mm1000 za mvua hupatikana katika Ukanda huu kwa mwaka.

(ii) Ukanda wa Tambarare:

Ukanda huu una mwinuko kati ya Meta 200 hadi Meta 400 kutoka Usawa wa Bahari na wastani wa mvua kwa mwaka ni mm 800 – 1,400. Ukanda umeenea karibu asilimia 25% (1,613.25km^2) ya eneo lote la Halmashauri.

Kwa ujumla Wilaya inapata nyuzi joto la 27^0C mpaka 39^0C kwa misimu mikuu mitatu ya hali ya hewa:-

(i) Msimu wa joto (Kuanzia mwezi Desemba – Machi)

(ii) Msimu wa Mvua (Kuanzia mwezi April – Mei)

(iii) Msimu wa Baridi (Juni – Septemba).

1.2 **MFUMO WA UTAWALA**.

Kiutawala Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ina Tarafa 6, Kata 21, Vijiji 91 na Vitongoji 775 vilivyosajiliwa katika Jimbo 1 la Uchaguzi la Handeni vijijini.

1.3 IDADI YA WATU NA MAKUNDI YA KIJAMII:

Idadi wa watu na makundi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka watu 73,508 mwaka 1957 na hata kufika mara mbili ya idadi ya watu wote kwa mwaka 2002 kwa idadi ya watu 200,356 (Wanaume 99,446 na Wanawake 100,910).

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya watu na Makazi ya Mwaka 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ilikuwa na watu 276,646 (wanaume 137,218 (49.60%) na wanawake 139,428 (50.40%). Kutokana na kasi ya ongezeko la watu kwa asilimia 3.3 kwa mwaka, kwa mwaka huu 2016 idadi ya watu inakisiwa kufikia 315,019 ambapo wanaume ni 156,667 na wanawake ni 158,352.

Msongamano wa watu ni 46 kwa kila km^2. Msongamano mkubwa upo kando ya barabara kuu na miji midogo ya Mkata, Kabuku, Segera/Michungwani na Kwedizinga.

IDADI YA WATU KIKATA KULINGANA NA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA 2012.

Na.	Kata	Idadi ya Watu		
		Jumla	Wanaume	Wanawake
1	Segera	23,445	11,505	11,940
2	Ndolwa	23,317	11,553	11,764
3	Mazingara	15,854	7,783	8,071
4	Kwamsisi	11,351	5,654	5,697
5	Kwasunga	8,257	4,107	4,150
6	Kwaluguru	11,354	5,593	5,754
7	Kwankonje	10,671	5,313	5,358
8	Kwachaga	10,438	5,126	5,312
9	Kang'ata	9,099	4,843	4,256
10	Sindeni	16,790	8,135	8,655
11	Misima	13,366	6,393	6,973
12	Kiva	9,972	4,895	5,077
13	Kabuku	12,222	5,939	6,283
14	Kwamatuku	11,219	5,794	5,425
15	Kwedizinga	6,319	3,180	3,139
16	Mgambo	11,317	6,121	5,196
17	Komkonga	16,262	7,850	8,412
18	Mkata	21,142	10,465	10,465
19	Kitumbi	10,737	5,315	5,422
20	Kabuku Ndani	15,551	7,787	7,764
21	Kwamgwe	7,970	4,125	3,845
	Total	**276,646**	**137,218**	**139,428**

Chanzo: *National Bureau of Statistics Census 2012*

2.0 DIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA HANDENI

Kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa matumizi bora ya rasilimali zilizopo na utawala bora (Educated community with access to improved and sustained social – economic services).

2.1 KAULI MBIU (MISSION STATEMENT)

Jamii iliyoelimika inayopata huduma za kijamii na kiuchumi zilizoboreshwa (To provide high quality social – economic services through effective use of available resources with good governance practices.)

2.2 MALENGO (OBJECTIVES)

Malengo ya ujumla ifikapo mwishoni mwa mwaka 2015 ni kama ifuatavyo:-

A. Kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi na kuboresha huduma kwa wenye Ukimwi na Virusi vya Ukimwi. (Improve services and reduce HIV/AIDS infection).

B. kuboresha utekelezaji wa sera ya kuzuia na kupambana na rushwa. (Enhance, sustain and effective implementation of the National Anti-corruption strategy).

C. kuboresha upatikanaji na utoaji wa huduma bora za kiuchumi na kijamii. (Improve access, quality and equitable social services delivery).

D. Kuongeza ubora na upatikanaji wa huduma za kijamii na miundombinu. (Increase quantity and quality of social services infrustructure).

E. kuboresha utawala bora na huduma za kiutawala. (Good governance and Administrative services enhanced).

F. kuboresha maisha bora, usawa wa kijinsia na kuiwezesha jamii. (Improve social welfare, gender and community empowerment).

G. Kuboresha na kuendeleza utunzaji wa maliasili na mazingira. (Management of Natural resources and environment enhanced and sustained)

H. Kuboresha tahadhari ya majanga na kuyakabili. (Emergency and disaster management improved).

I. Kuboresha maendeleo ya uchumi wa jamii. (Local economic development coordination enhanced).

2.3 SERA NA MIKAKATI:

Halmashauri ya Wilaya Handeni itafikia malengo/matarajio iliyojiwekea kwa;-

- kushirikisha Jamii katika kubuni, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini Miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa kwenye ngazi zote na kuhakikisha kuwa inaweka mikakati endelevu ya ukusanyaji wa mapato, ambayo

yatatumika kwa uangalifu na umakini wa hali ya juu ili yaweze kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi.

- Halmashauri ya Wilaya Handeni pia itaelimisha jamii kuhusu Sera mbalimbali za Kitaifa na umuhimu wa kutumia sheria ndogo zilizopo kuhakikisha kuwa shughuli zote zinazotekelezwa kwenye maeneo yao, zinafanyika kulingana na taratibu, kanuni na sheria zilizopo.
- Kushirikisha jamii katika kutekeleza miradi kwa nguvu zao wenyewe kwa njia mkabala bila kuathiri hali zao kiuchumi na kufikia malengo ya kuongeza wigo wa kutolea huduma za kijamii kama afya, elimu, uzalishaji na utawala bora.

3.0 HALI YA MAENDELEO KISEKTA:

Uchumi wa Wilaya ya Handeni umejikita sana katika Kilimo, Mifugo, Maliasili na Misitu. Shughuli za uzalishaji kupitia kilimo, ufugaji na misitu ndiyo chanzo kikuu cha kipato kwa wananchi wa Handeni. Kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya mwaka 2012, pato la mwananchi wa handeni kwa mwaka 2012/2013 lilikisiwa kuwa Tshs 810,000/- kwa mwaka. Lengo la Wilaya ni kuhakikisha kuwa pato la mkazi linaongezeka na kufikia shilingi 1,500,000 ifikapo mwaka 2021.

Asilimia 90 ya wakazi wote wa Halmashauri wanajishughulisha na Kilimo (Wakulima wadogo wadogo na wa kati) na asilimia 10 wamejiajiri katika biashara ndogondogo.

Katika kuinua uchumi wa mwananchi na kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuboresha huduma za kijamii, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni katika mipango yake ya maendeleo, imejiwekea kipaumbele katika mambo yafuatayo;-

- Elimu (Msingi na Sekondari) hususan kuinua taaluma,
- Ujenzi wa nyumba za watumishi,
- Kilimo cha kisasa na minada ya Mifugo,
- Kuboresha miundombinu ya Maji,
- Huduma za Afya na masuala mtambuka ya UKIMWI,
- Hifadhi ya mazingira,
- Kupambana na rushwa, na
- Jinsia na watoto.

3.1 Sekta ya Kilimo na Mifugo

Wananchi wa Handeni wanategemea sana shughuli ya kilimo cha mazao ya chakula, biashara na ufugaji. Kati ya watu 276,646 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, idadi ya nguvu kazi ni watu 151,652 ambao wanategemea kilimo na mifugo.

Eneo linalofaa kwa kilimo cha mazao mchanganyiko ni hekta 287,966 sawa na asilimia 41, na kati ya hizo kiasi kinachotumika ni hekta 161,639 sawa na asilimia 56.1. Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji zipo hekta 5,596 na zinazotumika ni hekta 50 sawa na asilimia 0.9. Hali kadhalika eneo linalofaa kwa malisho ni hekta 367,530 ambapo hekta 219,128 ndizo zinazotumika sawa na asilimia 60. Eneo lililotengwa kwa hifadhi ya misitu ni hekta 52,504 sawa na asilimia 7, kati ya hizo hekta 20,326 ni misitu ya

Serikali kuu, hekta 5,026 misitu ya Halmashauri na Hekta 27,152 ni misitu inayosimamiwa na Vijiji.

Zipo programu mbalimbali zinazotumika ili kukiwezesha kilimo kiwe cha tija ambazo ni mpango wa kuendeleza sekta ya kilimo (DADPs), Mradi wa kuongeza thamani ya mazao (MIVARF), Vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS), Vyama vya wakulima (AMCOS), Benki za maendeleo ya vijiji (VICOBA) na mifuko mingine ya uwezeshaji.

Halmashauri inahamasisha matumizi ya zana bora na pembejeo za kilimo. Wilaya ina jozi 549 za wanyamakazi, matrekta madogo 63 na matrekta makubwa yamefikia 87. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila Kata inakuwa na matrekta matano ifikapo mwaka 2021.

Aidha, kufunguka kwa barabara na uwepo wa masoko ya mazao ya chakula, biashara yakiwemo ufuta, matunda na alizeti, malisho ya mifugo na maeneo ya uwekezaji wa mashamba makubwa na ranchi ndogo ndogo. Aidha, Halmashauri imeendelea kuboresha masoko ya mazao ya kilimo na mifugo kwa kuongeza minada, vituo vya kukusanyia maziwa na kusindika mazao ya kilimo.

3.2 Hali ya chakula katika Wilaya

3.2.1 Utekelezaji wa malengo

Katika msimu wa mwaka 2015/16 wa uzalishaji wa mazao ya chakula, lengo lilikuwa kulima hekta 148,231 ili kuzalisha tani 317,049. Utekelezaji ni kwamba jumla ya hekta 134,630 zimelimwa ambazo zilitarajiwa kuzalisha tani 48,661 sawa na asilimia 36.

Hali hii ilitokana na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyosababishwa na mvua kunyesha kwa mtawanyiko mbaya na kwa muda mfupi iliyopelekea wakulima kuchelewa kupanda. (Aprili wakati msimu wa kupanda kila mwaka ni kati ya mwishoni mwa mwezi Februari na katikati ya Machi).

Katika msimu wa mwaka 2016/17 wa uzalishaji wa mazao ya chakula, lengo lilikuwa kulima hekta 157,244 ili kuzalisha tani 308,250. Utekelezaji ni kwamba jumla ya hekta 81,857 zimelimwa ambazo zilitarajiwa kuzalisha tani 100,715.

3.2.2 Hali ya chakula na bei sokoni 2016/2017

Hali ya chakula kwa mwaka 2016/17 ni nzuri. **Mahitaji halisi ya chakula kwa mwaka ni tani 84,390 na uzalishaji kwa mwaka 2016/2017 unatarajiwa kuwa tani 100,715 kwa hiyo wilaya inategemea kupata ziada ya tani 16,325.** Hali ya ongezeko la chakula inatokana na ongezeko la mvua za kutosha za vuli na masika kwa mwaka 2016/2017.

Bei ya vyakula katika soko la Handeni kwa sasa ukilinganisha na kipindi kama hiki kwa msimu uliopita 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

Zao	Bei kwa kilo 100 (Tshs) Msimu 2015/2016	Bei kwa kilo 100 (Tshs) Msimu wa 2016/2017

Mahindi	55,000 – 60,000	40,000 – 50,000
Maharage	150,000 – 180,000	180,000 – 200,000
Mchele	180,000 – 200,000	190,000 – 200,000
Kunde	130,000 – 180,000	100,000 – 110,000
Choroko	2,500 - 3,000	120,000 – 150,000
Mbaazi	80,000 – 100,000	90,00 - 120,000

Aidha katika kujikinga na upungufu wa chakula unaojitokeza mara kwa mara kutokana na mabadiliko ya tabia nchi Wilaya imefanya yafuatayo;-

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imetekeleza agizo la Mhe. Rais la kuanzisha kilimo cha Muhogo kwa kila kaya kupanda ekari moja, ili kuwa na uhakika wa chakula cha kutosheleza mwaka mzima kwa kila kaya.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mbegu bora ya muhogo aina ya Kiroba imenunuliwa na kusambazwa katika shule 57 za msingi na sekondari na kupandwa katika ekari 83.8 ili kuzalisha mbegu ambayo itasambazwa kwa wakulima wengi zaidi msimu ujao wa 2017/2018. Kata zilizonufaika ni Kiva, Mazingara, Mkata, Kitumbi, Ndolwa, Kabuku, Kabuku Ndani, Mgambo, Sindeni, Kwamatuku, Segera, Komkonga na Misima.

Vilevile Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo Shirika la WORLD VISION Tanzania wamesambaza mbegu ya muhogo katika kata 9 za Kwamsisi, Kwasunga, Segera Kwamgwe,na Kwedizinga, Kwachaga, Kwaluguru, Kwankonje na Kang'ata katika shule za msingi 35 na sekondari 9 ambapo jumla ekari 69.25 zimepandwa.

3.2.3 Mazao ya Biashara.

Mazao ya biashara yaliyolimwa msimu wa 2015/16 ni miembe, michungwa, alizeti, korosho na ufuta. Lengo lilikuwa kulima hekta 73,294.7 ili kuzalisha tani 408,866.7 na utekelezaji wake ni kuwa jumla ya hekta 59,500.9 zimelimwa na kuzalisha tani 215,817 sawa na asilimia 53 ya matarajio ya mavuno kama Jedwali hapa chini linavyofafanua.

Mazao	Malengo		Matarajio ya Utekelezaji		Asilimia
	Hekta	Tani	Hekta	Tani	
Miembe	2,327	27,924	2,128	23,408	83
Alizeti	9,329	13,994	4,643	13	0.3
Korosho	350	350	119.9	95.92	27
Korosho mpya	85.7	85.7	0	0	0
Michungwa	22,900	320,600	22,529	180,232	56
Pamba	256	256	60	60	23
Ufuta	38,047	45,657	30,021	12,008	26
Jumla	**73,294.7**	**408,866.7**	**59,500.9**	**215,817**	**53**

Kwa msimu wa mwaka 2016/2017 Mazao ya biashara yaliyolimwa ni Pamba, miembe, michungwa, alizeti, korosho na ufuta. Lengo lilikuwa kulima hekta 94,184 ili kuzalisha tani 68,111

3.2.4 Sekta ya Mifugo

Halmashauri imeanza mikakati mahususi ya kuendeleza sekta ya mifugo kwa kuwahusisha wafugaji wahamaji katika ufugaji wa kisasa unaozingatia ubora wa mifugo na malisho. Idadi ya mifugo katika sensa iliyofanyika mwaka 2016 ni kama ifuatavyo: wapo ng'ombe 131,842, mbuzi 110,176, kondoo 33,477, kuku 378,565, nguruwe 1,155, punda 1,372 na mbwa 8,124.

Lengo la uboreshaji wa mifugo ni kuhakikisha kuwa hadi ifikapo mwaka 2021 wananchi wawe na uwezo wa kuuza mifugo na nyama nje ya nchi, hii itabadilisha hali ya maisha kwa wafugaji na kuondokana na ufugaji wa kuhama hama.

Aidha, katika uboreshaji wa mifugo, yapo madume bora ya ngombe 820, mabeberu ya kisasa 600 na majogoo ya kisasa 1,650 ambayo yanatumika kwa ajili ya uboreshaji wa mifugo. Uhamilishaji ni njia nyingine inayotumika kuboresha ng'ombe, ambapo Halmashauri imejiwekea malengo ya kuhamilisha ng'ombe 2,000 kwa mwaka. Kwa mwaka 2016/2017 ng'ombe 500 wamehamilishwa.

Halmashauri ina vitalu vyenye ukubwa kati ya hekta 3,000 hadi 4,000 kila kimoja, pia imetenga maeneo kwa ajili ya kuanzisha ranchi za kijamii (community ranches) kwa ajili ya wafugaji wadogo. Kwa maana hiyo, tumewahimiza wamiliki wa vitalu kuweka sehemu ya kunenepeshea mifugo (feedlot ting) ili waweze kunenepesha mifugo ya wafugaji wa kawaida kwa maelewano maalum. Jedwali lifuatalo hapo chini linaonesha aina ya ranchi au vitalu vya wafugaji vilivyopo hapa wilayani.

Ranchi ya Taifa na Vitalu vya wafugaji

Aina ya ranchi/kitalu	Aina ya mifugo		
	Ng'ombe	**Mbuzi**	**Kondoo**
Mzeri Hill Ranchi (NARCO)	2,500	60	200
Nkale Ranchi	306	513	0
Olosipa farm	1,300	180	150
Sado farm	50	250	250
Major One farm	200	0	150
Shalom farm	400	0	0
Good chance farm	400	0	0
Mukuti farm	1,000	0	0
Stage farm	400	160	0
Klub Africo farm	120	0	0
Jumla	**6,676**	**1,163**	**750**

Eneo la malisho ni hekta 367,530 ambazo zina uwezo wa kulisha takriban ng'ombe 200,000. Hata hivyo eneo hilo linatumika kwa shughuli mbalimbali za kilimo, makazi na migodi hivyo kusababisha migogoro kati ya wafugaji na wadau wengine wanaotumia ardhi. Jitihada zinazoendelea ni kuainisha upya maeneo ya malisho kupitia mipango ya matumizi bora ya ardhi na hadi sasa Vijji 21 vimetengenezewa na kuainisha maeneo ya malisho katika mpango wa matumizi bora ya ardí, Lengo hadi 2025 likamilike vijiji vyote.

3.3. Ushirika na Maendeleo ya Jamii

Vyama vya Ushirika vilivyopo hadi kufikia Desemba 2016 ni 51. Kati ya hivyo zipo SACCOS 30, vyama vya Ushirika wa madini 4, Ushirika wa Maziwa 3 na Vyama vya wakulima na masoko (AMCOS) 14. Mikopo iliyotolewa kwa wanachama wa vyama wa wakulima imefikia thamani ya Shs. 1,177,147,151. Mikopo iliyorejeshwa ni Shs. 796,125,282.29 na ambayo haijarejeshwa ni Tshs 355,156,012.

Halmashauri imeendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali kupitia Mfuko wa Vijana na Wanawake kwa ajili ya kuendesha miradi midogomidogo. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri iliweza kutoa kiasi cha Tshs. 30,660,000/= kwa Vikundi 18 ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha Tshs. 26,660,000/= kilitolewa kwa Vikundi 15 vya Wanawake na kiasi cha Tshs. 4,000,000/= kwa Vikundi 3 vya Vijana kwa ajili ya kuendesha shughuli ndogondogo za ujasiriamali. Marejesho ya mikopo hiyo yataanza kufanyika mwaka fedha 2017/2018.

3.4. Sekta ya Ardhi na Maliasili

Halmashauri ina hifadhi ya misitu yenye hekta 52,504 (7%), kati ya hizo hekta 20,326 ni misitu ya Serikali kuu, hekta 5,026 misitu ya Halmashauri na hekta 27,152 ni misitu ya Vijiji. Wananchi kwa sasa wanashiriki katika utekelezaji wa sera ya hifadhi misitu mfano kijiji cha Gole kimeanza kuvuna msitu wao na kwa mwaka wa 2016/2017 na kinategemea kupata zaidi ya Tshs. Milioni 50 kwa maendeleo yao.

Shughuli za ufugaji nyuki ni mojawapo ya chanzo muhimu cha mapato ya kaya na hifadhi ya mazingira. Wilaya ina maeneo mazuri yanayofaa kwa ufugaji nyuki. Jumla ya vikundi 12 vinahusika na ufugaji nyuki vyenye wafugaji 700 wanaomiliki jumla ya mizinga 11,509 ikiwemo mizinga 755 ya kisasa na mizinga 10,754 ya kiasili. Kutokana na hali ya hewa kutokuwa nzuri uzalishaji wa asali umefikia lita 65,886 (kilo 92,830.09) kwa mwaka badala ya makisio ya lita 98,829 (kilo 139,245.135) na kilo moja ya asali inauzwa Shs. 10,000/=. Mpaka kufikia juni 2017 uzalishaji wa mazao ya nyuki yamefikia lita 220 sawa na thamani ya Tshs 3,099,690.34

Sekta ya ardhi inaendelea kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hii ambapo vijiji 41 vimeandaliwa na kukabidhiwa vyeti vya ardhi ya vijiji vinavyoonesha mipaka ya vijiji husika ili kusaidia utoaji wa hati miliki za kimila. Hadi kufikia Desemba 2015 jumla ya hati miliki 1,035 za kimila zimetolewa kwa wananchi. Kati ya vijiji 91 vilivyopo Halmashauri ya Handeni, vijiji 21 vina mipango ya matumizi bora ya ardhi..

3.5. Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko

Sekta hii ni miongoni mwa sekta zinazochangia ukuaji wa pato la mwananchi pamoja na Wilaya kwa ujumla. Halmashauri ya Wilaya haina kiwanda hata kimoja kinachofanya kazi ya uzalishaji na kuleta ajira kwa wananchi.

Aidha, biashara kubwa inayofanywa kwa sasa ni kupitia mazao ya chakula na biashara kupitia vyama vya ushirika wa wakulima (AMCOS) kwa kuuza mahindi kwa bei yenye tija kwa soko rasmi la kwa Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA)

Vile vile kwa bidhaa za mifugo Halmashauri imeendelea kuboresha minada na kuvutia wawekezaji ili waje kufungua viwanda vya bidhaa za mifugo kusafirisha nje ya nchi.

3.6 Sekta ya madini

Handeni inaongoza kwa kuwa na aina nyingi za madini katika Mkoa wa Tanga. Madini haya yanatumika katika shughuli za vito, ujenzi na kemikali viwandani. Ni malighafi muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi na Halmashauri.

Na	Kundi la Madini	Aina ya Madini	Mahali
01	Metallic Minerals	Gold	Magambazi, Kilimamzinga, Kang'ata, Kwedijava, Gole, Nyasa, Mtunguru, Suwa, Kwachaga, Bondo, Mjembe, Kwedijava, Kwamagome
		Copper	Mzundu, Kwamsangazi, Seza kofi, Magamba
		Iron ore	Lugala (Kitumbi)
02	Industrial Minerals	Dolomite	Mkata, Kwedikwazu, Seza kofi, Mzundu, Chogo, Mumbwi, Chanika Kofi
		Graphite	Mkalamo
		Marble	Seza kofi, Kitumbi
03	Gemstone	Blue garnet	Kingo, Kibindu
		Ruby	Kwasunga
		Aquimarine	Kwamsisi
		Reg garnet	Kwamsisi, Sezakofi, Kwamkunga
		Rhodolite	Chanika kofi, Seza kofi, Kwamkunga, Kwamagome, Imalange, Mkababu
		Tourmaline	Kwamsisi, Kibindu
		Spinal	Kwankoje
		Green garnet	Kwamkunga

3.7 Mawasiliano na nishati

Halmashauri ya Wilaya ina mitandao ya mawasiliano ya makampuni ya TTCL, Vodacom, Airtel, Zantel, Tigo, Halotel na Shirika la Posta.

Huduma za posta zinaendeshwa na kampuni ya Taifa ya Posta (Tanzania Postal Services Company Ltd. Pia zipo huduma za Fax na internet. Vile vile huduma za redio na luninga hupatikana kwa makampuni yote kutegemeana na aina ya king'amuzi anachomiliki mwananchi na serikali.

Ipo nishati ya umeme wa gridi ya Taifa ambao unapita katika vijiji vya pembezoni mwa barabara ya lami kutoka Korogwe hadi Handeni na Handeni hadi Mkata. Shirika la umeme (TANESCO) Wilaya ya Handeni linashughulika na kusambaza umeme katika vijiji vipya. Jumla ya vijiji 23 kati ya 91 vimewekewa umeme kupitia wakala wa umeme vijijini REA.

3.8 Mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF)

TASAF awamu ya tatu inajishughulisha na uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini, kuanzia mwezi Septemba 2015 kwa kutoa fedha kwa kaya 7,816 katika vijiji 54 kati ya

vijiji 91 vilivyopo. Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ni mojawapo kati ya Halmashauri 16 nchini ambazo zipo katika mpango wa tathimini (Impact Evaluation) hivyo mbali ya vijiji 65 ambavyo viliingizwa katika mpango huu vijiji 11 bado havijaanza kulipwa kwa vile vipo katika mpango wa tathimini (Impact Evaluation.)

Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Juni 2017 jumla ya Tshs 1,604,483,000/= zimelipwa kwa kaya maskini zilizopo katika vijiji 54 kama jedwali linavyoonesha hapo chini:-

MWEZI	KAYA ZILIZOLIPWA	KIASI KILICHOLIPWA	MAELEZO
JULY – AUG 2016	7,713	282,348,000	Kaya 147 hazikulipwa
SEPT – OCT 2016	7,798	283,755,000	Kaya 62 hazikulipwa
NOV – DEC 2016	7,775	277,268,000	Kaya 64 hazikulipwa
JAN – FEB 2017	7,194	258,600,000	Kaya 622 hazikulipwa
MAR – APR 2017	7,225	252,772,000	Kaya 591 hazikulipwa
MAY – JUNE 2017	7,190	249,740,000	Kaya 505 hazikulipwa
JUMLA		**1,604,483,000**	

Note: *kaya hizo ambazo hazikulipwa inatokana na sababu mbali mbali zikiwemo vifo, kuhama na kutotokea kabisa kwenye kituo cha malipo, Hivyo fedha zao kurejeshwa TASAF makao makuu baada ya kubakia.*

Mafanikio makubwa yameonekana kupitia mpango huu ambapo jumla ya Kaya 4,500 zimekubali kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya (CHF) baada ya kuhamasishwa, japokuwa kuna changamoto ya uhaba wa magari katika halmashauri yetu.

4.0 HUDUMA ZA JAMII

4.1.1 Elimu ya awali

Halmashauri ya Wilaya inaendesha elimu ya awali katika shule 118. Idadi ya wanafunzi wa elimu ya awali ni 8,090 (wav. 3,939 was. 4,151). Shule zote za msingi zina darasa la elimu ya awali, kwa sasa jitihada zinafanyika kwa ajili ya kuboresha miundombinu ikiwemo vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na madawati pamoja na kuongeza idadi ya walimu wenye sifa ya kufundisha elimu ya awali.

4.1.2 Elimu ya Msingi

Zipo shule 117 za serikali na 1 ya binafsi zenye jumla ya wanafunzi 77,908 (wav. 39,448 was. 38,460).

Kwa mwaka 2016 tulitarajia kuandikisha wanafunzi 7,401 wakiwemo (Wav 3,801 na Was 3,600) lakini tuliandikisha wanafunzi 16,445 (Wav 8774 na Was 7671) ongezeko hili ni sawa na asilimia 194.92 ambalo limetokana na mwitikio mkubwa wa wazazi kuwapeleka watoto wao shule kutokana na mpango wa utolewaji wa elimu bure.

Kwa mwaka 2017 tulitarajia kuandikisha wanafunzi wa Elimu ya awali 9,955 (Wav 4,920 na Was 5,035), hadi kufikia mwezi Aprili uandikishwaji ni 9,473 kati yao wav 4,642 was 4,831 sawa na 95%. Aidha kwa upande wa darasa la kwanza lengo ni kuandikisha 9,995 wakiwemo wav 4,920 na was 5,035 hadi kufikia mwezi Aprili uandikishaji ni 14,558 kati yao wav 7,425 was 7,133 sawa na asilimia 146% Hii imetokana na mwitikio

mkubwa wa wazazi kuwapeleka watoto wao shule kutokana na mpango wa Serikali wa kutoa elimu msingi bila malipo.

Halmashauri ya wilaya ya Handeni kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 ilipokea fedha za elimu bure Tshs 362,730,000 na Posho ya madaraka kwa walimu wakuu kiasi cha Tshs 343,800,000. Kwa upande wa miondombinu ya madawati Halmashauri ilikua na upungufu wa madawati 25,000 mpaka kufikia mwezi juni 2016 kulikua na jumla ya madawti 25017 ikiwa ni ziada ya madawati 17.

4.1.3 Kiwango cha taaluma

Kiwango cha taaluma kimepanda kutoka asilimia 72.6 katika mtihani wa Taifa darasa la saba mwaka 2014 hadi asilimia 77 mwaka 2016. Kiwango hicho kinatokana na wanafunzi 4,082 waliofaulu mtihani wa Kitaifa mwaka 2016 (wav. 1,704 was. 2,378). Mafanikio haya yametokana na juhudi za ufundishaji wa walimu, wanafunzi kujituma katika kujifunza, upatikanaji wa chakula cha mchana, udhibiti wa utoro, mchango wa wazazi na wadau wengine wa elimu.

4.1.4 Hali ya utoro shuleni

Hadi kufikia Mei 2017 utoro wa wanafunzi ulipungua na kufikia wanafunzi 162 sawa na asilima 0.2, na hakukuwa na mimba sawa na asilimia 0. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwarudisha wanafunzi waliotoroka shuleni. Mafanikio yameonekana baada ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa dhidi ya wazazi na walezi wanaowaozesha watoto wa shule ikiwa ni pamoja na kuwapeleka mahakamani.

4.1.5 Elimu ya watu wazima

Vipo vituo 22 vya MEMKWA na MUKEJA vyenye jumla ya washiriki wa kundi rika la kwanza na la pili wapatao 273 (Me. 145 Ke 128). Vipo vituo vya ufundi stadi 3 (Sindeni, Kabuku, Kwamkono) na Elimu masafa ina washiriki 7 wengi hujitokeza wakati kunapokaribia kipindi cha mitihani.

4.2 Elimu ya Sekondari

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ina shule za sekondari 24 (23 za Serikali na shule 1 ya binafsi). Shule hizi kwa mwaka huu 2017 zina idadi ya wanafunzi ni 6,932 (wav. 3,211 na was. 3,721). Mahitaji ya walimu wa sekondari kwa sasa ni 651 waliopo ni 504 (Me 343 na Ke161). upungufu ni 147 ambapo uhaba mkubwa wa walimu ni katika masomo ya hisabati na sayansi. Kwa walimu wa sayansi waliopo ni walimu 79 (Me 57 na Ke 22) Uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ni 1:53 ambapo uwino kisera ni 1:40.

4.2.1 Ujenzi wa vyumba vya maabara za Sekondari na Samani.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imejenga vyumba 69 vya maabara, vyumba 4 vimekemilika kwa 100%, vyumba 3 vinakamilishwa ifikapo Agosti mwaka huu 2017 na vyumba 62 vipo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Halmashauri inashukuru kwa kupatiwa vifaa vya maadara katika sekondari 5 kati ya 23 za Serikali. Inaomba shule zilizosalia zipatiwe vifaa vya maadara ili kuborosha ufundishaji wa masomo ya sayansi.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imetekeleza agizo la Mhe. Rais; la kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anakuwa na dawati. Kabla ya agizo kulikuwa na upungufu wa meza 1017 na viti 1345. Halmashauri imekarabati meza 830 na kutengeneza mpya 187 na hivyo kuondoa upungufu wa meza. Kwa upande wa viti Halmashauri imetengeneza viti vipya 150 na kukarabati 1195 hivyo kumaliza tatizo la upungufu wa viti. Halmashauri Haina upungufu wa meza na viti katika shule za sekondari.

4.2.2 Mapambano dhidi ya utoro na mimba

Hali ya utoro na mimba katika shule za sekondari imepungua. Mwaka huu 2017 mimba 2 zimeripotiwa ukilinganisha na mimba 5 wakati kama huu mwaka 2016. Mahudhurio ya wanafunzi na utoro wa rejareja nao umepungua kwa mwaka 2015 utoro ulikuwa 15% mwaka huu 2017 ni 10% hii imetokana na mafanikio ya elimu bila malipo kwas hule za sekondari. Aidha katika kupambana na tatizo la utoro na mimba Halmashauri ipo katika ujenzi wa bweni la wanafunzi shule ya sekondari Kisaza ambapo kiasi cha Tshs. 50,000,000.00 zimepelekwa kusaidia ujenzi huo hadi kukamilika kwa kutumia nguvukazi ya Jeshi la Kujenga Taifa – Mgambo.

4.2.3 Kiwango cha taaluma

Ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha IV unaimarika ambapo kwa mwaka 2014 ufaulu ulikuwa 57%, mwaka 2015 ni 62.5% na mwaka 2016 umeongezeka hadi 66% ambapo wanafunzi waliofanya mtihani ni 1,255 (wav 623 na was 632), wanafunzi 789 wav 409 na was 379 wamefaulu kwa daraja la kwanza hadi la tatu kati yao wanafunzi 168 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka huu 2017. Lengo ni kuongeza ufaulu kutoka 66% mwaka 2016 hadi 76% mwaka 2017

4.3 Sekta ya Afya

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ina vituo vya kutolea huduma za afya 44. Vituo hivyo ni Hospitali 1 St Francis Kwamkono (FBO) vituo vya afya 2 ambavyo vinamilikiwa na serikali. Zahanati zipo 41 kati ya hizo 37 ni za serikali na 4 ni za binafsi (1 FBO na 3 watu binafsi).

4.3.1 Huduma ya afya ya uzazi na mtoto

Mpaka Disemba mwaka 2016 vifo vya watoto chini ya miaka 5 vilikuwa 1 kwa kila 1,000 hii ni hatua kubwa katika kupunguza vifo vya watoto ikilinganishwa na vifo 34 kwa kila 1,000 mwaka 2012. Vifo vya mama wajawazito kwa kila vizazi hai 100,000 vimepungua kutoka 284 mwaka 2012 hadi kufikia 146 Disemba 2016. Matarajio ya wilaya ni kupunguza vifo hivyo hadi kufikia 84 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo Disemba 2019.

Huduma ya chanjo kwa mama na mtoto anapozaliwa hasa homa ya manjano na pepopunda inatolewa katika vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya. Sehemu ambazo hakuna vituo vya kutolea huduma za afya, chanjo hutolewa kwa njia ya wima na mkoba. Upatikanaji wa chanjo ni 100% kwa sasa na uwiano wa watoto waliochanjwa umeongezeka kutoka 84% 2015 hadi 100% mwaka 2016.

4.3.2 Mapambano dhidi ya UKIMWI

Ukubwa wa tatizo la maambukizi ya virusi vya ukimwi katika Wilaya umepungua kutoka 3.7% mwaka 2009 hadi 2.8% Disemba 2016.

Huduma za matunzo na tiba kwa wanaoishi na VVU zinatolewa katika vituo 5 ambavyo ni kituo cha afya St. Francis Kwamkono, Kituo cha afya Kabuku, Kituo cha afya Mkata, Zahanati ya segera na zahanati ya Mgambo-JKT. Pia huduma hiyo inatolewa kwa njia ya mkoba katika zahanati 12 na wataalamu kutoka hospitali ya Wilaya ya Handeni. Wanufaika wa huduma hii ni watu 3,138 kati ya hao wanawake 2,211 na wanaume 927.

Huduma za upimaji wa VVU pamoja na huduma za kuzuia maambukizi ya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto hutolewa katika vituo vyote vya Umma.

4.3.3 Mapambano dhidi ya malaria

Ugonjwa wa malaria bado ni tatizo ingawa maambukizi na hata vifo vimepungua. Maambukizi yamepungua kutoka 29% mwaka 2013 hadi 11% mwaka 2016 na vifo vitokanavyo na malaria vimepungua kutoka 1.9% mwaka 2013 hadi 0.2% mwaka 2016.

4.3.4 Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba

Pamoja na kuongezeka kwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kununua dawa na vifaa tiba kutoka Tshs. 818,212,263 (2013/14) hadi Tshs. 1,147,356,922 (2016/17) kumekuwepo na changamoto ya upatikanaji wa dawa muhimu kutoka bohari ya dawa MSD kwa baadhi ya vipindi pia fedha zinazotengwa kwenye bajeti kutopatikana kama ilivyopangwa.

Uanzishwaji wa bohari ndogo ya dawa na vifaa tiba ya Halmashauri imelenga kurahisisha upatikanaji wa dawa muhimu kwa muda mfupi na kupunguza uhaba wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mpango huu kwa asilimia 100 unategemea fedha zinazokusanywa katika vituo vya huduma za afya, kuhakikisha dawa muhimu na vifaa vinakuwepo wakati wote ndani ya halmashauri.

4.3.5 Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

Mpaka Juni 2017 kaya wanachama hai ni 31,600 kati ya kaya lengwa 52,303, sawa na asilimia 60%. Muitikio wa wananchi kujiunga na mfuko unaongezeka kutokana na juhudi za uhamasishaji unaofanyika kuanzia ngazi ya vijiji mpaka wilayani. Wanachama wa CHF wameongezeka kutoka 20,907(31%) julai 2016 hadi 31,600 (60%) juni 2017. Jumla ya fedha Tshs 420,720,000/= zilikusanya ambapo Tshs 266,330,000/= ni fedha za michango ya kaya na Tshs 154,390,000/= ni malipo ya Tele kwa Tele.

4.3.6 Dirisha la wazee

Halmashauri ya Wilaya yetu ina wazee waliokwishatambuliwa 17,259 ikiwa 8,868 ni wanawake na 8,391 ni wanaume. Wazee hawa wote hupatiwa matibabu bure kupitia dirisha la wazee katika vituo vyote vya serikali na wazee 4,500 wameshapatiwa vitambulisho ambapo kati ya hao 1,950 wana kadi za CHF. Halmashauri ya wilaya ya

Handeni imeweka utaratibu wa kila kijiji kuchangia gharama za matibabu kwa wazee Tshs.200,000/= kwa mwaka ili kupunguza pengo la fidia ya huduma zinazotolewa kwa msamaha. Hadi Julai 2017 ni vijiji vinne (4.4%) kati ya vijiji 91 vimetoa mchango huo, sawa na Tshs 800,000/=.

4.3.7 Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM)

Wilaya imeendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa huduma za afya zinapatikana karibu na jamii kwa kuongeza na kuimarisha miundombinu ya zahanati, vituo vya afya, hospitali na ujenzi wa nyumba za watumishi. Hadi kufikia Julai 2017, zipo zahanati 41, vituo vya afya 2 na hospital 1 (FBO). Idadi ya vituo vinavyoendelea kujengwa ni zahanati 13, kituo cha afya 1 na Hospitali 1.
Juhudi nyingine zinazofanyika ni uboreshaji wa vituo vya afya vilivyopo ili kuviwezesha kufanya upasuaji tukilenga zaidi huduma za dharura za uzazi. Tumeanza na kituo cha afya Mkata ambapo wodi ya kisasa ya wazazi imekamilika na jengo la upasuaji lipo katika hatua ya umaliziaji.
Zahanati 2 ujenzi umekamilika lakini hazijaanza kutoa huduma kwa sababu ya uhaba wa watoa huduma. Uhaba wa watumishi ni changamoto kubwa katika kutoa huduma za afya. Jumla ya zahanati 17 kati ya 36 za serikali hazina tabibu, sawa na asilimia 47%. Upungufu wa watumishi ni kwa asilimia 75 hasa kada muhimu za tabibu, daktari na uuguzi.

Ufanisi unaopatikana katika uboreshaji wa huduma za Afya unatokana na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika Halmashauri kwa kupitia vyombo vifuatavyo;

a) Kamati ya usimamizi wa huduma za Afya Wilayani (CHMT)
b) Bodi ya huduma za Afya Wilayani
c) Kamati zilizoundwa kwa mifumo ya Halmashauri
    - Elimu, Afya na Maji
    - Kamati ya UKIMWI Wilaya
    - Kamati za Afya za Kata/Vijiji

4.4 Huduma za Maji

Upatikanaji wa huduma ya maji katika Halmashauri ya Wilaya Handeni umeongezeka kutoka asilimia 52 kwa mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 59.3 mwaka 2016. Vyanzo mbalimbali vya maji vilivyopo katika Wilaya ya Handeni ni pamoja na visima vifupi na virefu, visima vya kienyeji, mabwawa, uvunaji wa maji ya mvua kwenye mapaa ya nyumba na skimu ya maji Handeni Trunk Main (HTM).

4.4.1 Hatua mbali mbali zinazochukuliwa kukabiliana na tatizo la maji.

Halmashauri ya Wilaya Handeni iliingia mikataba ya Ujenzi wa Mabwawa matatu (3) ya Maji katika vijiji vya Manga, Mkata, na Kwandugwa kwa mwaka wa Fedha 2013/2014. Utekelezaji wa Miradi hii Haujakamilika kutokana na Miradi hii kujengwa chini ya kiwango, ambao umetokana na Usanifu duni, Usimamizi hafifu na ujenzi usiuokua na weledi.

Vyanzo vya maji vinavyotumiwa na wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ni Mradi wa maji wa HTM ambao unahudumia vijiji vipatavyo 66, Mradi wa maji Chalinze ambao unahudumia kijiji 1, Mabwawa Madogo ambayo hukusanya maji ya Mvua, Visima Vifupi, Visima Virefu na Uvunaji wa maji ya mvua kutoka katika mapaa ya nyumba.

Aidha ili kuendelea kupunguza tatizo la upatikananji maji Halmashauri ya Wilaya Handeni inaendelea na uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora za bati ili kuweza kuvuna maji ya mvua, pia Wilaya ya Handeni imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali katika kutatua kero ya maji.

4.4.2 Changamoto zinazoikabili sekta ya maji.

Changamoto zinazoikabili sekta ya maji ni pamoja na uchakavu wa mitambo ya kusukumia maji na miundombinu yake, ukosefu wa vyanzo vya maji vya uhakika, ukosefu wa fedha za kufanyia ukarabati wa baadhi ya miradi iliyobomoka kutokana na mvua, gharama kubwa ya matengenezo, ongezeko la watu na mifugo ambalo limeongeza uhitaji wa maji, Maji yaliyochini ya ardhi ambayo hupatikana kwa njia za visima kuwa na chumvi nyingi hivyo kuhitaji ‘‘Reverse Osmosis (RO) process’’ ili kuyafanya kuwa salama kwa matumizi ya binadamu. na kutokuwepo kwa usafiri kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji.

4.5 Barabara

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ina mtandao wa barabara wenye jumla ya urefu wa Km 820 ambazo zimegawanyika kama ifuatavyo Km 91 ni barabara kuu (kitaifa) ni za lami na zinahudumiwa na TANROADS, Km 166 ni barabara za Mkoa (km 111 lami na km 55 changarawe) hizi pia zinahudumiwa na wakala wa barabara TANROADS na km 563 ni barabara za wilaya na vijiji ambazo zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Changamoto kubwa inayokabili ni fedha kidogo zinazotolewa na mfuko wa barabara kwa ajili ya ukarabati ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi. Miundombinu ya barabara ni kiungo kikuu cha ukuaji wa uchumi kwa ajili ya usafiri na usafirisha wa bidhaa.

4.7 Huduma za Benki na Fedha

Huduma za Kibenki hutolewa na Micro-Finance Bank (NMB) iliyopo Handeni mjini na tawi jipya la Mkata, Tawi la Posta ambapo huduma hutolewa kwa wateja wanaoweka, kuchukua na kutuma fedha nje ya Halmashauri. Aidha, huduma za kifedha pia zinafanywa kwa njia ya simu.

Benki ya CRDB inatoa huduma zake za kuweka na kuchukua kupitia tawi jipya lililopo Handeni Mjini. Tunategemea huduma hii itaendelea kupanuka na kufika miji inayokuwa sana kibiashara ya Kabuku na Mkata, na kukuza sekta za kiuchumi za Kilimo, Biashara na Madini.

5.0: MASUALA MUHIMU (KEY ISSUES)

Wilaya ya Handeni imebaini mambo muhimu yakushughulikia:-

- Upatikanaji wa watumishi wa kutosha na kuwaendeleza kitaalam na ujuzi.
- Kuboresha huduma za afya kwa ujumla pamoja na wagonjwa wa Ukimwi.
- Kuboresha mazingira ya utendaji kazi na upatikanaji wa vifaa vya kufanyia kazi.
- Kuwajengea uwezo wananchi katika upangaji, usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- Ushirikishwaji wa wadau wa maendeleo(mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na sekta binafsi) katika mchakato wa maendeleo.
- Kuamsha ari ya wananchi katika kuchangia maendeleo yao.
- Kuimarisha mawasiliano na upashanaji habari baina ya wadau na sekta.
- Kuboresha miundombinu ya kijamii na kiuchumi.
- Kuhifadhi mazingira, matumizi bora ya ardhi na utunzaji wa vyanzo vya maji.
- Kuweka tahadhali katika kukabiliana na majanga mbalimbali kama mafuriko.
- Kuimarisha usimamizi wa Sheria Ndogo za Halmashauri.

6.0: HITIMISHO

Karibuni sana handeni tuweze kushirikiana kuleta maendeleo kwa wananchi kupitia fursa za uwekezaji wa sekta ya mifugo na kilimo, vilevile madini ya ujenzi na vito pia.

.....
WILLIAM M. MAKUFWE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HANDENI